

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO**

Simu: 022 2126826  
Nukushi: 022 2126834  
Tovuti: [www.habari.go.tz](http://www.habari.go.tz)  
Barua pepe: [km@habari.go.tz](mailto:km@habari.go.tz)



Mji wa Serikali  
Mtaa wa Habari,  
S. L. P. 25,  
Mtumba,  
40481 DODOMA.

**SALAMU ZA POLE**

**TAARIFA KWA UMMA**

**Aprili 1, 2020 Dodoma.**

Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Dkt. Harrison Mwakyembe (Mb) ametoa pole kwa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Habari Tanzania (TBC) Dkt. Ayub Rioba kwa kuondokewa na Mwanahabari Nguli Bw. Marin Hassan Marin leo asubuhi Jijini Dar es Salaam.

Akiongea moja kwa moja na televisheni ya TBC 1, Dkt. Mwakyembe ameeleza kuwa TBC na tasnia ya habari kwa ujumla imepata pigo kwani Bw. Marin alikuwa mstari wa mbele kuhakikisha sekta ya Habari inakuwa na mchango chanya katika maendeleo ya jamii.

Enzi za uhai wake marehemu alikuwa mmoja wa waasisi wa vipindi kadhaa vya TBC vikiwemo Jambo Tanzania, Nyumba ya Jirani na Aridhio.

Dkt. Mwakyembe ametoa pole kwa familia, ndugu, jamaa, marafiki na wadau wote wa tasnia ya habari nchini.

Imetolewa na

Lorietha Laurence  
Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini,  
Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.